



Taarifa kwa vyombo nya habari
Imezuiliwa hadi tarehe 23 Aprili, 2014

Wananchi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara wanataka uwajibikaji zaidi

Wengi wangeipigia kura ya ndiyo rasimu ya sasa ya katiba

23 Aprili 2014, Dar es Salaam: Mjadala katika Bunge la Katiba umejaa na ubishi na mgawanyiko, lakini Watanzania wameungana kutaka katiba yenyewe uwajibikaji zaidi kwa viongozi wa umma na mfumo wa utawala wenye uwazi zaidi. Mionganoni mwa vifungu katika rasimu pili ya katiba ambavyo vinaungwa mkono na wananchi walau sita kati ya kumi ni:

- Idadi kubwa ya Watanzania wanaunga mkono vifungu vinavyohusiana na haki ya wananchi kupata taarifa au habari, na kuongezeka kwa uwajibikaji na uwazi wa viongozi wa umma
- Mapendekezo kwa ajili ya utaratibu wa kudhibiti na kuwajibisha wabunge na mgawanyo wa madaraka ili kuepuka migogoro ya kimaslahi yanaungwa mkono na wengi

Matokeo haya yametolewa na Twaweza kwenye muhtasari wa utafiti wenye jina la "*Je, Watanzania wanafikiri nini hasa juu ya katiba?*" Matokeo ya utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa. Muhtasari umetokana na takwimu kutoka *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa uliofanyika kote Tanzania Bara, na *Wasemavyo Wazanzibari*, Utafiti kwa njia ya simu ya mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa uliofanyika visiwani Zanzibar, ukiendeshwa na Taasisi ya Kimataifa ya Sera na Sheria (The International Law and Policy Institute).

Sauti za Wananchi imebaini kuwa, uungwaji mkono ni mkubwa sana mionganoni mwa wananchi wa Tanzania Bara kwenye vifungu vingi viliviyowasilishwa katika rasimu ya kwanza ya katiba na vimebaki katika rasimu ya pili. Vifungu hivyo ni vile vinavyohusu kuwepo kwa uwajibikaji zaidi kwa watumishi wa umma, kuimarisha utaratibu wa dola ili kudhibiti na kuwajibisha wabunge, hasa wabunge kuwajibika kwa wapiga kura wao, na kuongeza ushindani zaidi wa kisiasa.

Utafiti pia unaonesha kuwa Watanzania wangeipitisha rasimu ya katiba bila shida ikiwa Watanzania sita kati ya kumi wameonesha kuwa wangeipigia kura ya Ndiyo. Tanzania Bara ni wananchi asilimia 65 na Zanzibar ni wananchi asilimia 62 wanaoikubali rasimu ya sasa.

Hata hivyo, suala la muundo wa serikali bado ni tata. Idadi kubwa ya Wazanzibari (80%) walisema wanataka muundo wa serikali tatu, ikilinganishwa na chini kidogo ya nusu (43%) ya wahojiwa kutoka Tanzania Bara. Aidha, zaidi ya nusu ya wahojiwa kutoka Zanzibar (53%) walisema kuwa uungaji mkono wa rasimu ya sasa ya katiba utategemea muundo wa serikali tatu.

Sauti za Wananchi na *Wasemavyo Wazanzibari* pia ziligundua kuwa wananchi kutoka Tanzania Bara wamepata fursa kufuatilia midahalo na mijadala ya katiba mpya. Wananchi sita kati ya kumi (62%) kutoka Bara wamekuwa wakifuatilia kwenye radio, luninga au mijadala ya wazi, wakati wenzao wa Zanzibar, ni wananchi watatu tu kati ya kumi (30%) ndiyo wamefanya hivyo.

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema "*Idadi kubwa ya Watanzania wanakubaliana katika masuala muhimu kwenye katiba - serikali kuwa na uwazi zaidi, na viongozi wa umma kuwajibika. Ingawa suala la muungano bado ni tata, pengine suala la serikali mbili au tatu linaweza kufikiriwa kwa kutafakari athari zake kwenyemasuala muhimu kwa watu.*

Aliongeza, "Uongozi wa kweli siyo kutetea kwa nguvu msimamo na maslahi yako mwenyewe, lakini kudadisi mitazamo na maoni mbalimbali, na kujenga makubaliano mapya kulingana na kanuni za msingi na maslahi ya pamoja."

---- mwisho ----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Risha Chande

Meneja Mawasiliano, Twaweza

Baruapepe: rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 657559

Maelezo kwa Wahariri

- Muhtasari huu na takwimu zilizomo zinapatikana hapa www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayomlenga raia na inayokusudia kuleta mabadiliko makubwa Afrika Mashariki. Twaweza inaamaini kwamba mabadiliko ya kudumu hayana budi kuanzia chini kwenda juu. Tumedhamiria kujenga mazingira na kupanua fursa ambazo zitatoa mwanya kwa mamilioni ya watu kuhabarishwa and kuwawezesha kuweza kuleta maendeleo katika jamii zao moja kwa moja na kuifanya serikali iwajibike.
- Unaweza kufuutilia kazi za Twaweza kupitia:
Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza_NiSisi